***MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI***

# TANGAZO KWA UMMA NA WADAU WA UCHUNGUZI WA VINASABA VYA BINADAMU (PATERNITY TEST)

[***Chini ya Sheria ya "Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu" ya 2009, Sura ya 73***]

## A. UTARATIBU WA KUCHUKUA SAMPULI

### *A.1. Utaratibu wa kuchukua sampuli za Vinasaba ukoje kisheria:*

Utaratibu wa kuchukua sampuli kwa ajili ya Kipimo cha Vinasaba (DNA) umeelekezwa kutegemeana na mambo yafuatayo:

(a) Aina ya shauri (jinai au "paternity")
(b) Taasisi husika na Mamlaka hitaji (Requesting – Authority)
(c) Aina ya sampuli
(d) Nani mhusika wa kipimo
(e) Gharama
(f) Mawasiliano

### *A.2. Nani anayeruhusiwa kuchukua sampuli kisheria?*

Sheria ya Vinasaba vya Binadamu imewataja wanaoruhusiwa kuchukua sampuli za Vinasaba kuwa ni:

(a) Wakemia walioteuliwa na Waziri mwenye dhaman aya Afya na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.
(b) Askari wa Jeshi la Polisi mwenye cheo kuanzia Inspekta, au
(c) Daktari aliyesajiliwa kutoka hospitali inayotambulika na Serikali.

## B. MAOMBI YA UCHUNGUZI WA VINASABA

### *B.1. Nani anastahili kuleta maombi ya kufanyiwa uchunguzi:*

Ni lazima mashauri yote ya kuhitaji kufanyiwa kipimo cha Vinasaba yapitie kwenye moja kati ya Mamlaka/Taasisi zifuatazo kutegemeana na aina ya shauri.

(a) Jeshi la Polisi
(b) Mahakama

(c) Ustawi wa Jamii/Manispaa au Mkuu wa Wilaya
(d) Hospitali teule/binafsi zilizosajiliwa na Serikali.
(e) Wakili wa kujitegemea
(f) Vituo vya utafiti vilivyosajiliwa

***B.2. Nani ni mhusika wa kufanyiwa kipimo cha uchunguzi:***

Kipimo kitahusisha wote waliotajwa katika barua inayowasilishwa na Mamlaka hitaji kama vile Baba, Mama na Mtoto, na Baba/Mama na Mtoto/Watoto.

**C. GHARAMA ZA KIPIMO CHA UCHUNGUZI WA VINASABA**

Gharama za uchunguzi kwa kila mmoja huwa ni shilingi ***LAKI MOJA TU*** (TSHS. 100,000/=)

**D. UFUATILIAJI NA UCHUKUAJI WA MATOKEO YA UCHUNGUZI WA VINASABA**

(a) Kabla na baada ya uchunguzi: Mwakilishi au Mhusika kutoka Mamlaka/Taasisi iliyohitaji kufanyika kwa uchunguzi (Requesting Authority) ndiye ataruhusiwa kufuatilia.
(b) Mtu yeyote aliyeombewa vipimo na mamlaka hitaji haruhusiwi kufuatilia matokeo ya uchunguzi.

**E. UPOKEAJI WA MATOKEO YA UCHUNGUZI**

(a) Mwakilishi au Mhusika kutoka Mamlaka/Taasisi iliyohitaji kufanyika kwa uchunguzi (“Requesting Authority”) ndiye anayestahili kupokea matokeo ya uchunguzi wa vinasaba, na si vinginevyo.
(b) Mamlaka husika itawajibika kutunza matokeo hayo kwa usiri mkubwa na kuheshimu barua ya matokeo.

**F. UWASILISHAJI WA TAARIFA YA MATOKEO YA UCHUNGUZI WA VINASABA KWA MTEJA.**

Kwa kuzingatia umakini na usiri mkubwa unaohitajika, taratibu zifuatazo zizingatiwe:

(a) Utoaji wa maelezo ya matokeo ya uchunguzi ufanyike kwa wahusika wote kwa pamoja wakiwepo.

(b) Nakala ya ripoti ya matokeo ya uchunguzi itolewe kwa wahusika wote waliofanyiwa kipimo bila kubagua.
(c) Maelezo ya matokeo ya uchunguzi kwa wahusika yatolewe kwa kuzingatia ustawi wa mtoto/watoto.
(d) Kama taasisi hitaji haina wataalam wa kuelezea matokeo hayo kwa mteja/wateja wao, basi wafanye mawasiliano na maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kabla ya kutoa maelezo hayo.
(e) Matokeo ya uchunguzi yapokelewe kwa taratibu za kiofisi (muhuri na sahihi ya ofisi husika) kabla ya kutolewa nakala yoyote.

## G. INAPOTOKEA MMOJA WA WAZAZI HAJARIDHIKA NA MATOKEO

(a) Awasilishe malalamiko yake kwa mamlaka/taasisi iliyohitaji kufanyika kwa uchunguzi na siyo yeye kutuma malalamiko kwa Mkemia Mkuu wa Serikali
(b) Taasisi/Mamlaka ikipokea malalamiko iwasiliane na Mkemia Mkuu wa Serikali, kwa kuwa wao ndiyo wanaojua upana wa tatizo la familia/kesi husika.

## H. VINASABA NI NINI?

(a) Vinasaba (DNA) ni chembechembe ndogo ambazo hubeba taarifa zote za kibailogia ambazo hutumika katika ukuaji na ufanyaji kazi wa kiumbe hai.
(b) Vinasaba ndivyo hubeba taarifa zote za kiumbe hai mfano: rangi yake ya ngozi, kimo chake, nywele zake, magonjwa ya asili ya kurithi n.k
(c) DNA hubeba taarifa muhimu za urithi wa binaadam, kwa mfano, magonjwa tabia na maumbile. Taarifa hizi zinaweza kutumika vibaya na waajiri, watu wa bima na hata katika masomo.
(d) Kila mtu ana vinasaba vyake ambavyo havifanani na mwingine ila isipokuwa kwa mapacha wawili wa yai moja.
(e) Vinasaba huweza kupatikana kutoka eneo lolote la mwili wa binadamu, mfano damu, mate, ngozi, mifupa, n.k.
(f) Pia wataalamu wa vinasaba hutumia mpanguso wa ndani wa kinywa ili kupata vinasaba kwa sababu ni njia rahisi, isiyo ya maumivu, hufanyika haraka na hata uhifadhi wake huwa ni rahisi.

## I. MIFANO YA MATOKEO YA UCHUNGUZI WA VINASABA VYABINADAMU

(a) Matokeo ya uchunguzi wa vinasaba yanahusiha ulinganishaji wa mpangilio wa chembechembe asili za urithi ("DNA Profile") zitokazo kwa baba kwenda kwa mtoto, na pia mpangilio wa chembechembe asili za urithi ("DNA Profile") zitokazo kwa mama kwenda kwa mtoto

(b) Matokeo yaulinganishaji wa mpangilio wa chembechembe asili za urithi ("DNA Profile") zitokazo kwa mtuhumiwa/mwathirika kufananishwa na profile zitokazo kwenye eneo la tukio.

(c) Hivyo tarakimu zinazoonekana kwenye barua ya matokeo ya uchunguzi zinasaidia katika ulinganishaji wa mpangilio wa chembechembe asili za urithi ("DNA Profile") ya wahusika.

## J. MFANO MWEPESI WA ULINGANISHI WA UHALALI WA MZAZI NA MTOTO

### *J.1. Mtoto akiwa ni wa Baba*

| ENEO (DNA) VINASABA | BABA | MTOTO | MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA BABA |
|---|---|---|---|---|---|
| **D8S1179** | 13, 14 | 13, 15 | 11, 15 | 15 | 13 |
| **D21S11** | 30.2, 31.2 | 28, 30.2 | 28, 30 | 28 | 30.2 |
| **D7SO20** | 11, 12 | 8, 11 | 8, 10 | 8 | 11 |
| **CSF1PO** | 10, 11 | 9,10 | 9, 11 | 9 | 11 |

### *J.2. Mtoto akiwa si wa Baba*

| ENEO (DNA) VINASABA | BABA | MTOTO | MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA BABA |
|---|---|---|---|---|---|
| **D8S1179** | 14, 16 | 13, 15 | 11, 15 | 15 | 0 |
| **D21S11** | 29, 29 | 28, 30.2 | 28, 30 | 28 | 0 |
| **D7SO20** | 9, 10 | 8, 11 | 8, 10 | 8 | 0 |
| **CSF1PO** | 12, 13 | 9, 10 | 9,10 | 9 au 10 | 0 |

### *J.3. Mtoto akiwa si wa Mama wala si wa Baba*

| ENEO (DNA) VINASABA | BABA | MTOTO | MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA BABA |
|---|---|---|---|---|---|
| **D8S1179** | 13,14 | 18, 15 | 20, 22 | 0 | 0 |
| **D21S11** | 30, 31 | 28, 32 | 14, 17 | 0 | 0 |
| **D7SO20** | 9, 10 | 10, 13 | 22, 16 | 0 | 0 |
| **CSF1PO** | 12, 14 | 19,20 | 8, 11 | 0 | 0 |

### *J.4. Mfano wachangamoto taratibu za ulinganishi*

(a) Kawaida Mama ndiye anaye anza kulinganishwa na mtoto; ikiwa maeneo yamebeba mpangilio unaolingana

| ENEO (DNA) VINASABA | BABA | MTOTO | MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA BABA |
|---|---|---|---|---|---|
| **CSF1PO** | 10, 12 | 11, 12 | 10, 12 | 12 | 0 |

(b) Japo kuwa Baba na Mama wote wana mpangilio wa 12, ni mama ambaye ataanza kuhusishwa na mtoto. Hivyo basi, eneo la baba linalooanishwa na mtoto ni lile la 10 tu ambalo mtoto hana.

| ENEO (DNA) VINASABA | BABA | MTOTO | MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA MAMA | MAENEO YA MTOTO YALIOOANA NA BABA |
|---|---|---|---|---|---|
| **D8** | 12,13 | 13,13 | 11,13 | 13 | 13 |

(c) Baba na mama wote wana mpangilio wa 13; pamoja na kuwa mama ndiye anayeanza kuhusishwa na mtoto; kwa mfano, huu kwakuwa mtoto anampangilio wa13,13, hivyo basi, eneo la baba linalooanishwa na mtoto pia ni la 13.

**Imetolewa na**

***MKEMIA MKUU WA SERIKALI***